

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

(Barua ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Telegram: Halmashauri

Simu: 026 269 2301

Simu: 026 269 2349

Fax : 026 269 2349

E-Mail Address

[md@nzegadc.go.tz](mailto:md@nzegadc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S. L. P 4,

NZEGA - MKOA WA TABORA

Unapojibu nukuu

Kumb.Na. NDC/CC.7/9VOL.II/67

04 April, 2018

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzege alipokea kibali cha ajira mbadala kwa watendaji wa Vijiji kwa barua ya tarehe 08 Machi, 2018 yenye Kumb.Na FA170/533/01/51 kutoka kwa katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

kwahiyo anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kujaza nafasi 51 za watendaji wa vijiji na nafasi 06 za watendaji wa kata

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI (VILLAGE EXECUTIVE) DARAJA LA III- (TGS.B). NAFASI (51)

#### a) SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo astashahada/cheti (certificate) katika moja ya fani zifuatazo:-Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo -Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### B. KAZI/MAJUKUMU

- i. Mtendaji na mshauri wa Halmashauri ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo ya kijamii na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.
- ii. Afisa masuuli na mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
- iii. Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iv. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- v. Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji.
- vi. Kutafsiri Sera, Utaratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogondogo za Halmashauri katika Kijiji.
- vii. Kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika kijiji chake na kuziwasilisha kwenye Kata.
- viii. Kuongoza vikao vya maendeleo ya Kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- ix. Kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa nia, umaskini na kuongeza uzalishaji.

- x. Kusimamia matumizi bora ya nguvu kazi.
- xi. Kiongozi wa wakuu wa vitengo wa kitaalamu katika Kijiji.

### C. MSHAHARA

**Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara wa Serikali yaani TGS B**

#### 2. MTENDAJI WA KATA (WARD EXECUTIVE) DARAJA LA II- (TGS.B). NAFASI (06) - STASHAHADA

##### b) SIFA ZA MWOMBAJI


- ii. Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo stashahada (Diploma) katika moja ya fani zifuatazo:-Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo -Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### NGAZI YA MSHAHARA TGS C

##### A. SIFA ZA JUMLA

- a) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- b) Waombaji wote wawe Watanzania .
- c) Waombaji wote waambatanishe nakala za cheti cha kuzaliw.
- d) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya Kidato cha nne na sita kwa wale waliopata kiwango hicho cha elimu na vyeti kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- e) Picha moja, passport size iandikwe jina la mhusika kwa nyuma.
- f) Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**statement of results havitakubalika**) wao
- g) Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **WASIOMBE KAZI** na wanapaswa kuzingatia maelezo yaliyo katika Waraka Na. **CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010**.
- h) Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya Posta au moja kwa moja Masijala ya Mkurugenzi kabla au ifikapo tarehe **17 April, 2018** saa tisa na nusu alasili kwa anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Nzega,  
S.L.P 4 - NZEGA**



**Jacob J. Mtalitinya  
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,  
NZEGA.**

**MKURUGENZI . MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
NZEGA.**